Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

JARIDA LA CoForEST
Toleo la 1 | Mei 2020

# OR-TAMISEMI yaahidi kutoa ushirikiano katika utekelezaji wa mradi wa Uhifadhi wa Misitu (CoForEST)



*Mkurugenzi wa Uratibu wa Sekta katika OR-TAMISEMI, Dkt Andrew Komba akiwa na wataalamu kutoka OR-TAMISEMI na waandamizi kutoka Idara mbalimbali pamoja na wawakilishi wa TFCG na MJUMITA katika picha ya pamoja baada ya kupata maelezo ya Mradi mpya wa CoForEST mjini Dodoma mwezi Februari 2020.*

"Tunawakaribisha sana wadau kama TFCG na MJUMITA, tunaratibu wadau wote katika mikoa na wilaya ili watekeleze shughuli zao vizuri. Tunafurahi kuona juhudi za kuimarisha ushirikiano wa utendaji wa kazi na OR-TAMISEMI". ….“tuko tayari na tuna nia ya kufanya kazi na kushirikiana nanyi. Wataalamu wetu wote watakuwepo kutoa ushirikiano katika mchakato wote wa kuandaa mikakati ya utekelezaji wa shughuli za mradi huu muhimu kwa jamii, misitu na Halmashauri zetu", aliongezea Dkt Komba kutoka OR-TAMISEMI.

Haya yalisemwa wakati timu kutoka TFCG na MJUMITA walivyoenda kuutambulisha mradi wa CoForEST rasmi kwa TAMISEMI mapema mwanzoni mwa mwaka huu.

"Miradi mingi ya maliasili imekuwa ikijikita sana kwenye dhana ya ulinzi tu bila kuangalia watu wanaoilinda wananufaika vipi na rasilimali hii, lakini kupitia dhana hii ya mradi wa CoForEST inaonesha mfumo utakaoleta tija katika uhifadhi kwa kuvuna kwa njia endelevu lakini na kulinda misitu vilevile" alisema Ndugu George Miringay, Afisa Ardhi Mwandamizi baada ya kuielewa dhana ya Uvunaji endelevu.

Wakichambua faida za mfumo wa usimamizi unaotumika na TFCG na MJUMITA, Watalamu walilinganisha mfumo huu kwa kutumia nadharia ya kisayansi inayo itwa 'Alternative Stable' ambayo inafaa kuelezea namna misitu ya miombo inavyorejea baada ya kukatwa na kuchipua na kuwa imara zaidi hivyo kuipa sifa za ziada za uhifadhi endelevu.

Umuhimu wa TAMISEMI kuwa sehemu ya huu mradi ni pale inapotoa mwongozo kutokana na kwamba kuna mgongano wa maslahi wa namna ardhi za vijiji na rasilimali zake zinaposimamiwa. Kwa hekta za misitu takriban milioni 48.1 zilizopo nchini, vijiji vingi vinahitaji kupata motisha ya kuendelea kusimamia asilimia 46% ya misitu inayopatikana kwenye ardhi za vijiji. Kuna ushindani mkubwa sana wa ardhi ya vijiji unaochangia ukataji wa miti. Ili kuweza kuinusuru misitu hii, hatuna budi kuwapa motisha jamii inayoishi kandokando mwa misitu hii kuendelea kulinda badala ya kuikata au kuigeuza mashamba. Ushirikiano na OR-TAMISEMI utajikita katika kutoa mwelekeo wa namna shughuli za mradi zinavyoweza kuenezwa wilaya nyingine, kuweka mazingira wezeshi ya kusaidia biashara endelevu ya mazao ya misitu kufanyika katika USM, na kusaidia jamii kuongeza thamani kwenye misitu.

## Ndani:

- OR–TAMISEMI yaahidi kutoa ushirikiano utekelezaji wa mradi wa Uhifadhi wa Misitu (CoForEST)
- Ujue Mradi mpya wa CoForEST
- Waheshimiwa Wabunge wapewa Elimu ya Misitu Bungeni
- Mradi wafanya ufuatiiaji katika maeneo yaliyofyekwa
- Vijiji na Wilaya vyachambuliwa kubaini vigezo





# Mradi wa kuhifadhi misitu kwa kuwezesha biashara endelevu ya mazao ya misitu Tanzania- (CoForEST)

Misitu ya asili ina mchango mkubwa sana katika maendeleo endelevu, kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Mwaka 2012, kulikuwa na hekta milioni ~32 za misitu na misitu ya miombo nchini. Pamoja na umuhimu wa misitu hii, inafyekwa hovyo kwa kiwango cha asilimia ~1.3 kwa mwaka. Upotevu mwingi wa misitu unafanyika kwenye ardhi za vijiji ambao husababishwa na mahitaji ya ardhi kwa ajili ya kilimo.

Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USM) ni nyenzo ya kisera ya usimamizi wa misitu iliyoundwa kuendeleza usimamizi endelevu wa misitu iliyoko kwenye ardhi za vijiji.

## Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii unamaanisha nini?

Nchini Tanzania, katika Sheria ya Misitu Namba 14 ya mwaka 2002, jamii ina haki ya kuanzisha Hifadhi ya Msitu wa Kijiji. Jamii inakuwa na kujumu la kusimamia msitu huo wa Kijiji na wanaweza kukusanya na kubakiza mapato ya mazao ya misitu ndani ya Kijiji. Mapato kutokana na vibali vya uvunaji yanatumika kulipia usimamizi wa msitu husika na miradi ya maendeleo ya jamii.

## Je, biashara endelevu ya mazao ya misitu ni nini?

Mfumo wa uvunaji unaotumika na Mradi wa CoForEST unalenga kuendeleza bioanuwai na mifumo mingine ya ikolojia inayopatikana katika misitu ya asili. Kwa kuunganisha uwelewa wetu wa ikolojia ya misitu aina ya miombo, kanuni za kisayansi za mbinu za misitu, mradi umeonyesha namna uvunaji endelevu wa mbao na mkaa unavyoweza kufanyika kwa njia endelevu katika misitu ya Hifadhi za Vijiji. Baada ya eneo kuvunwa uchipuaji asilia wa miti iliyovunwa inahamasishwa kupitia usimamizi na uangalizi makini dhidi ya usimamizi wa moto na kudhibiti shughuli nyingine kama uvamizi wa mifugo na kilimo.

Tangu mwaka 2012, watekelezaji wa mradi wa Kuleta Mageuzi Katika Sekta ya Mkaa Tanzania walifanikiwa kutekeleza mfumo wa USMJ ambao unajumuisha uzalishaji endelevu wa mazao ya misitu ya mkaa na mbao katika vijiji 35 Mkoa wa Morogoro. Mradi umeonyesha mafanikio katika kuboresha usimamizi wa misitu, ajira vijijini, na miradi ya maendeleo ya jamii

**Lengo kuu la mradi wa CoForEST:** Kuimarisha usimamizi endelevu wa misitu ya asili unaozingatia mabadiliko ya kiuchumi na utawala wa mazao ya misitu katika mnyonyoro wa thamani wa mazao ya misitu na kuchangia kukabiliana na kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

Mradi wa CoForEST umeundwa ili kuchangia dira ya maendeleo endelevu ya Tanzania kwa kuwezesha minyororo ya thamani ya mazao ya misitu nchini ikiwemo mkaa na mbao. Mradi unatarajia kufikia malengo yake kupitia matokeo matatu yanayohusiana:

### Tokeo la 1: Kuendeleza shughuli za USMJ na Kufanyia majaribio mfumo wa uwezeshaji wa USMJ

Uwezo wa mamlaka katika ngazi ya taifa, mkoa, na wilaya na wanajamii umeimarishwa ili kutekeleza na kupanua shughuli za USM katika njia ambazo zitaongeza shughuli mbalimbali za kuongeza kipato na kupunguza ukataji hovyo wa miti.



### Tokeo la 2: Kuongeza mjadala kuhusu uwepo wa sera na sheria wezeshi za USMJ na biashara endelevu ya mazao ya misitu

Uwepo wa sera na sheria wezeshi na mfumo endelevu wa uwezeshaji kwa ajili ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii na biashara endelevu ya mazao ya misitu.

### Tokeo la 3: Utafiti, Ufuatiliaji na Kujifunza

Taasisi za Utafiti na Mafunzo nchini Tanzania zinatoa taarifa na ujuzi mpya kuhusu biashara endelevu ya mazao ya misitu katika Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii, na kuingiza katika mfumo wa mafunzo ya wanafunzi.

## Eneo la Mradi wa CoForEST

Mradi utatekelezwa katika ngazi ya kitaifa kwa kuzingatia uwezeshwaji wa Halmashauri za Wilaya kwa ajili ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii katika Wilaya saba ambazo ni: Kilosa, Morogoro na Mvomero katika Mkoa wa Morogoro; Liwale, Ruangwa na Nachingwea katika Mkoa wa Lindi na Wilaya ya Kilolo katika Mkoa wa Iringa.



*Wanafunzi kutoka Kijiji cha Matuli, Morogoro, moja ya shule za msingi ndani vijiji zilizonufaika na mradi wa TTCS kupitia vijiji kuwezesha umeme shuleni, na kuwalipia wanafunzi gharama zingine kwa ajili ya masomo ya ziada.*

## Muda wa Utekelezaji wa Mradi

Mradi wa CoForEST utatekelezwa kwa miaka mitatu kutoka Desemba 2019 hadi Novemba 2022. Mradi wa CoForEST unaendeleza shughuli za mradi wa Kuleta Mageuzi katika Sekta ya Mkaa Tanzania (2012 – 2019).


Hata hivyo, utekelezaji wa mradi huu utachangia moja kwa moja katika dira ya Maendeleo ya nchi yetu kwa kuwezesha uwepo wa uendelevu katika mnyoror wa thamani wa mazao ya misitu hususan mkaa na mbao.

# Kuendeleza Usimamizi Shirikishi wa Misitu na Mipango ya Matumizi bora ya Ardhi

- **Vijiji 30 vya andaa na kutekeleza mipango ya misitu na ya ardhi**
- **Mchakato wa kurasimisha misitu ya vijiji wafikia pazuri kwa vijiji 30**
- **Alama za mipaka 2161 za simikwa kwenye mipaka ya misitu ya vijiji**
- **Ramani za mipaka za sajiliwa Wizarani**
- **Wananchi 298 wajengewa uwezo**

Ili msitu wa Kijiji uweze kutambulika na serikali, unapaswa kupitia mchakato unaoelekezwa kwenye Sheria ya Mistu Na. 14, kifungu cha 33 hadi 35. Hata hivyo, kupitia mradi wa TTCS, vijiji vyote 30 vilipata fursa ya kupitia mchakato huu ambao ni shirikishi.

Katika Wilaya ya Morogoro na Mvomero, misitu ya vijiji vya mradi 30 ilifanyiwa mchakato wa Kupitia upya mipaka ya misitu. Lengo likiwa ni kuwezesha misitu hii kupata sifa ya kutangazwa chini ya sheria. Hatua hii ilipelekea mipaka ya misitu hiyo kuweka mawe yenye alama (beacons) kwenye misitu ya vijiji 30 na mipaka ya misitu ya vijiji kusafishwa; Ramani za mipaka 30 zimetayarishwa na kupitishwa na Wizara ya Maliasili na Utalii.



*Ramani ya Matumizi Bora ya Ardhi ya Kijiji cha Chabima, ikionyesha Ramani iliyosajiliwa (JB) kwa ajili ya Msitu wa Hifadhi wa Kijiji cha Chabima.*

Aidha kule Kilosa, mipaka ya misitu ya vijiji 20 ilipitiwa upya kwa lengo la kupata sifa za kuja kutagazwa kwa misitu hiyo. Takribani mawe yenye alama 2,161 yalisimikwa kwenye mipaka ya misitu ya hifadhi ya vijiji 20. Ramani 56 za kusajili mipaka (JB maps) zimekwisha andaliwa na kusajiliwa katika Wizara ya Maliasili na Utalii.

- Nyaraka zinazotakiwa kukamilika ni pamoja na mipango ya Usimamizi wa misitu iliyopitiwa upya na yenye ramani za JB
- Mihutasari ya vijiji ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya Kijiji na Mkutano mkuu wa Kijiji.
- Taarifa za fedha za mwaka (miaka ya hivi karibuni)
- Na barua maalum kwenda kwa Mkurugenzi

## Kujengea uwezo wananachi kupitia Mafunzo mbalimbali

Watekelezaji wa mradi wa TTCS wamewajengea uwezo kupitia mafunzo ya namna ya kutekeleza mipango ya usimamizi bora wa radhi ya vijiji na mipango ya usimamizi wa misitu. Mafunzo kwa Halmashauri za vijiji, Kamati za Maliasili na Kamati za VLUM pamoja na wazalishaji wa mkaa na mbao kwa njia endelevu.

**Mafunzo kwa timu za doria-** Wananchi 298 wakiwemo wanawake 92 na wanaume 206 kutoka vijiji 30 vya mradi wakijumuisha Kamati za maliasili na timu za doria walijengewa uwezo kupitia mafunzo kwa timu za doria kuhusu mbinu za kufanya doria, utawala bora, usimamizi wa fedha na mapato ya vijiji ikiwa Pamoja na namna ya kusimamia mapato yanayokusanywa na kijiji kwa kutumia vitabu rahisi vya kumbukumbu na kuwasilisha taarifa mara kwa mara katika Ofisi ya Wilaya, upambanaji na uzuiaji wa moto, mbinu za usalama kazini, na namna ya kukabiliana na wahalifu Pamoja na hatua za kuchukua, namna ya kufanya vikao na mikutano, kuweka kumbukumbu. Mafunzo haya yalitolewa na Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Jamii cha Likuyu Sekamaganga. Vijiji vilivyonufaika ni Kamati za Maliasili kutoka vijiji 10 vya Mbamba, Chabima, Kisongwe, Unone, Mvumi, Zombo - Lumbo, Madizini, Gongwe, Mfuluni and Rudewa Gongoni Kutoka Kilosa na Kamati za maliasili kutoka vijiji vya Maharaka, Sewekipera, Kihondo, Misengele and Msongozi Wilayani Mvomero na vijiji vya Mlilingwa, Diguzi, Matuli, Lulongwe and Tununguo Wilayani Morogoro zilipatiwa mafunzo ya usimamizi wa misitu na masuala ya utawala bora wakati huo huo timu zao za doria zilipewa mafunzo kuhusu: namna ya kupunguza ukataji wa miti (upotevu wa misitu), kufanya doria msituni, mbinu za kupambana na moto na Mbinu za Usalama kazini

### Zaidi ya Hekta 141,610 za misitu ya vijiji za hifadhiwa

Tangu mwaka 2012 hadi 2019, Wilaya tatu Mkoani Morogoro yaani Kilosa, Morogoro na Mvomero zilinufaika kwa utekelezaji wa Mradi wa Kuleta Mageuzi katika Sekta ya mkaa Tanzania (TTCS). Kupitia shughuli zake, hadi kufika mwisho wa mwaka 2019, vijiji 30 vilikuwa vimefikiwa na shughuli za mradi kupitia dhana ya kuingiza uvunaji endelevu wa mazao ya misitu (mkaa na mbao) katika Usimamizi wa Misitu ya Vijiji. Vijiji hivi viliingiza dhana hii katika mipango ya usimamizi wa misitu yao. Aidha, kufikia mwishoni mwaka 2019, hekta zaidi ya 141,610 ya misitu ya matajiwazi (miombo) ilikuwa imeingizwa kwenye utataribu wa hifadhi za misitu kwenye ardhi za vijiji katika vijiji 30 ndani ya Wilaya ya Morogoro, Kiosa and Mvomero.




## Waheshimiwa Wabunge wapewa semina ya Uhifadhi wa Misitu-Wahamasishwa kuunga mkono USM

Ofisi ya Bunge kupitia Mradi wao wa Kujengea Uwezo Wabunge Awamu ya Pili iliandaa semina kwa ajili ya Waheshimiwa kutoka TAPAFE yaani Chama cha Marafiki wa Mazingira kutoka Bungeni, na Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, pamoja na Kamati ya Bunge ya Viwanda Biashara na Mazingira. Semina hii ilifanyika katika viwanja vya Bunge Tarehe 18 Aprili 2020 ikiwa na lengo la kuongeza uwelewa miongoni mwa waheshimiwa wabunge na kuwajengea uwezo wa kuchambua fursa, changamoto na manufaa ya masuala yanayohusu misitu nchini. Wakati wa kufungua semina hii, Mgeni Rasmi Mheshimiwa Hassan Zungu (MB) aliesimama katika picha ambae pia ni Waziri wa Nchi, Muungano na Mazingira, alionyesha wasiwasi wake juu ya kiwango kikubwa cha upotevu wa rasilimali ya misitu ambacho kinachangiwa sana na shughuli za maendeleo, Wizara yake ina jukumu la kuhakikisha hali hii haiendelei kwa kushirikisha wadau wote pamoja na jamii.

Hata hivyo, Mheshimiwa Zungu alitambua kwamba kiasi kukubwa cha upotevu wa misitu kinatokana na shughuli zisizoendelevu za kilimo zinazoendelea katika maeneo mengi kupelekea kiwango cha ukataji wa mitu kuongezeka mithiri ya kupoteza hekta 469,000 za misitu kwa mwaka nchini.

Pamoja na kuhamasisha watu kutumia nishati mbadala ya gesi ili kuinusuru misitu, waheshimiwa wabunge waliomba serikali kuhakikisha inapunguza kodi kwa vifaa na bidhaa za gesi na nishati nyingine ili wananchi waweze kumudu gharama yake.

Katika semina hii, mada mbili kuu ziliwasilishwa na wakuu wa Taasisi hizi kutoka Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) Bw. Charles Meshack pamoja na Kamishna wa Uhifadhi kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Profesa Dos Santos Silayo.



Katika wasilisho la Mkurugenzi wa TFCG kwa wabunge, alisistiza kuwa kuendeleza misitu iliyoko kwenye ardhi za vijiji kuna faida nyingi ikiwemo za mifumo ikolojia na kuhimili mabadiliko ya tabia nchi; kama hakuna juhudi za makusudi hazitofanyika na kuacha hali kama ilivyo kwa sasa, misitu iliyoko kwenye ardhi za vijiji itagezwa kuwa mashamba miaka 30-40 ijayo; Usimamizi shirikishi wa misitu unaweza kupunguza kiwango cha ufyekaji wa misitu; kuweka misitu yote katika mamlaka moja ya usimamizi kunaweza kuongeza hatari ya migogoro na kuongezeka kwa upotevu wa misitu na kupunguza mapato; ni wakati sasa kuunga mkono usimamizi Shirikishi wa Misitu na kuhamasisha vijiji vyote vyenye misitu kuanzisha misitu ya vijiji.



*Mheshimiwa Jitu Soni, Mwenyekiti wa Chama cha Marafiki wa Mazingira Bungeni (TAPAFE), Mhes. Dkt Ishengoma, Prof Dos Santos pamoja na Mkurugenzi wa TFCG Dkt Meshack katika picha ya pamoja baada ya semina ya wabunge.*



Aidha Prof Dos Santos Silayo katika mada yake alikuwa anaangazia namna Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) pamoja na changamoto zilizopo juhudi zinazofamyika kuongoa maeneo ya misitu yaliyoharibika; hii ni pamoja na upandaji wa miti, uanzishwaji wa mashamba mapya, utekelezaji wa sheria, na udhibiti wa matumizi ya mazao ya misitu.

Hata hivyo waheshimiwa wabunge walihimizwa kutetea misitu wakiwa wanachangia Bungeni kama moja ya njia ya kuelimisha. Pamoja na hayo, wengi walisisitiza utunzaji na ufuatiliaji wa miti  inayopandwa ili juhudi hizi ziwe na tija.

**Baadhi ya Maoni ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu misitu –**

“Serikali na wadau wawe na mikakati ya kuwezesha kila mwanafunzi kupanda mti na kuutunza hadi ukue kuanzia shule za msingi, hii utasaidia kuwa na kizazi kinachopenda mazingira”, alisema Mheshimiwa Maganga Ndassa R.I.P (MB) .

Mheshimiwa Kiluswa (MB) alitoa ushauri kuhusu uanzishwaji wa mamlaka, “ili kupunguza sintofahamu katika uanzishwaji wa mamlaka hii ya misitu ni vyema Wakala wa Huduma za Misitu na Idara ya Misitu na Nyuki kuhakikisha kila hatua ya uundaji ishirikishe na kupata maoni ya na wadau katika ngazi zote, kwa namna hii hata changamato za utekelezaji wake zitakuwa zimetafutiwa ufumbuzi katika mchakato huu” alisisitiza.

“TFS hawataweza kutatua changamoto za misitu bila kushirikisha wadau muhimu na sekta husika, hivyo ili kutatua mkanganyiko wa utekelezaji wa sera mbalimbali, sekta zote na wadau muhimu washirikishwe kuandaa mikakati ya kupunguza changamto hizi” alisema Mheshimiwa Lorensia (MB).

“Watunga Sera wanatakiwa kutambua kwamba ili kutatua changamoto ya mahitaji ya nishati ya kupikia nchini, tunahitaji kuwa na mikakati tofauti inayosaidiana kuchangia mahitaji hayo kutokana na hali halisi ya nchi yetu na teknolojia tuliyonayo. Tunahitaji miongozo ya namna nishati mbalimbali ikiwemo ya mkaa na kuni zitakavyosimamiwa, na uwekezaji unaotakiwa na kwa muda gani” alisema Charles Meshack Mkurugenzi Mtendaji wa TFCG.

“Ili kuongeza hamasa na ushawishi, kila mbunge ajitahidi kuchangia mawazo ya kuboresha sekta ya misitu wakiwa ndani ya Bunge, tunaahidi ushirikiano kwa wadau ili kuchangia mazingira wezeshi ya kusimamia misitu ya asili” alisema Mheshimiwa Jitu Soni (MB) na Mwenyekiti wa TAPAFE wakati wa kuhitimisha warsha.

# WATALAAMU WACHAMBUA VIGEZO, VIJIJI, NA WILAYA ZA KUTEKELEZA MRADI WA CoForEST

Watalamu wa mradi wa CoForEST walijumuika na Kitengo cha Uratibu wa Sekta, kinachoshughulikia Maliasili na Mabadiliko ya Tabia Nchi kutoka TAMISEMI, Wataalamu wa Maliasili Mikoa, Wataalamu wa Ofisi za Maliasili za Wilaya ili kufanya uchambuzi yakinifu wa Wilaya na vijiji na kuutambulisha mradi, kuelezea malengo yake vigezo vya kuchagua wilaya na vijiji vya kutekeleza mradi na shughuli zake pamoja na mikakati ya uendelevu. Timu ilienda kimkakati, katika Wilaya zilizotembelewa ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi, Handeni, Rufiji, Liwale, Kilwa, Kilolo, Nachingwea.

Baada ya kutembelea na kujadiliana na watalaam kuhusu vigezo, changamoto, hatari, utayari pamoja na kuchambua hali ya misitu katika wilaya zote, timu ilikubaliana na kuridhika na vigezo vilivyofikiwa na Halmashauri za Wilaya za Kilolo, Handeni, Liwale na Nachingwea. Wilaya zote zina kiwango cha misitu kinachofaa kwa ajili ya kutekeleza mfumo wa mradi, pamoja na kuwa na misitu ya kutosha, wilaya hizi zilionyesha utayari wa kutekeleza mfumo za kuingiza dhana ya uzalishaji wa mkaa na mbao kwa njia endelevu katika Hifadhi za Misitu ya Vijiji. Zoezi hili pia lilipata ushiriki kutoka kwa ofisi za Wakurugenzi wa Wilaya, Washauri wa maliasili Mkoa, Wakuu wa Wilaya, na RAS.

*Wataalam wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale wakijadiliana kuhusu vigezo mbalimbali ikiwemo kupata taarifa za misitu ndani ya Wilaya. Vijiji vya Nambinda, Mlembwe na Mpengele vilionekana kuwa na sifa za kutekeleza mradi ndani ya Wilaya ya Liwale*





*Timu ya Watalamu ikiongozwa na Mshauri wa Maliasili Mkoa wa Tanga Ndugu Sosiya, wakiwa na Afisa Misitu Ndugu Adam Sylivester, watumishi wa TFCG pamoja na viongozi wa vijiji kutoka Kijiji cha Maligwa, Wilaya ya Kilindi walipotembelea Msitu wa Kijiji cha Maligwa.*

# Kijiji cha Mahenge, Wilayani Kilolo

- **Wataalamu wa Wilaya ya Kilolo wasaidia kutoa na kuchambua vigezo**
- **Usimamizi Shirikishi wa Misitu ni kigezo kimoja wapo**

Mwanzoni mwa mwezi Machi 2020, timu ya wataalamu wa mradi kwa kushirikiana na timu ya wataalam kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, walitembelea Mkoa wa Iringa katika Wilaya ya Kilolo kwenye vijiji vya Ikula, Mahenge, Udekwa na Mgolowe kwa dhumuni la kutembelea maeneo ya misitu ya vijiji kama inafikia vigezo vya kutekeleza mradi wa mkaa endelevu na kuongea na uongozi wa vijiji husika.

Wajumbe walio shiriki kwenye ziara hii ya kutembelea vijiji katika Wilaya ya Iringa ni Afisa Ardhi wa Wilaya, Afisa Misitu wa Wilaya, Afisa Mtendaji wa Kata, viongozi wa husika na wawakilishi kutoka Kamati za Maliasili za kila Kijiji. Viongozi wa vijiji husika walihusishwa kupitia mikutano maalum ya uelimishaji na kwa njia shirikishi. Njia na vifaa mbalimbali kama vifaa vya GPS, simu janja zenye uwezo wa kupokea ramani maalum.



*Sehemu ya msitu wa Kijiji cha Ikula, Wilaya ya Kilolo, moja ya vijiji vilivyotembelewa wakati wa kuchambua vigezo vya vijiji vya kutekeleza mradi.*



## Je wakijua Kijiji cha Mahenge?

Kijiji cha Mehenge kinapatikana upande wa Kaskazini mwa Wilaya ya Kilolo barabara ya kwenda Dar es Salaam kutoka Iringa. Ni makao makuu ya Tarafa na Kata ya Mahenge. Kijiji kina ukubwa wa hekta 17,689 na idadi ya watu kiasi cha 2,318 wakiwemo wanawake 1249 na wanaume 1069. Kijiji kina vitongoji vinne ambavyo ni Kibotola, Lungumba, Mlewela na Mlowe. Kijiji kina hati ya usajili wa Kijiji.

Pamoja na kuwa na Kamati ya Matumizi bora ya ardhi, na Kamati ya Maliasili vinavyoshirikiana na Halmashauri ya Kijiji. Kuna chumba kimoja cha Ofisi ambacho kinatumika kwa shughuli zote za serikali. Utekelezaji wa shughuli za kamati hizi ungekuwa bora zaidi kama wangepatiwa mafunzo ya majukumu yao ili kuwekeza kwenye ushirikiano mzuri uliopo baina ya uongozi wa Kijiji na wananchi wake. Kilimo cha mbogamboga kama nyanya, na ufugaji ndo shughuli kuu za kiuchumi. Baadhi ya wananchi wanafanya shughuli za misitu hususan mkaa na mbao na wengi wao wanafanya kinyume cha sheria.

## Aina ya Misitu ya Kijiji cha Mahenge

Kuna aina nyingi za misitu katika Kijiji. Kuna miombo, misitu ya milimani, na misitu ya Savana. Kijiji kimetenga eneo la Hifadhi ya Msitu wa Kijiji. Misitu mingine haijahifadhiwa. Kuna misitu mingine iko chini ya Halmashauri ya Wilaya. Changamoto kubwa kwenye misitu ni uvamizi kwa ajili ya kufungua mashamba, uchimbaji wa madini pamoja na ufugaji ndani ya Hifadhi za misitu. Hata hivyo, Kijiji cha Mahenge kina eneo kubwa la misitu ya miombo kwenye ukanda wa chini ambao unafaa kwa utekelezaji wa mradi. Miti ya mbao pia ipo na kwa utaratibu wa uvunaji.



*Sehemu ya Msitu wa Kijiji cha Mahenge, Kilolo*

# WANAVIJIJI WILAYA ZA KILOSA, MOROGORO NA MVOMERO WAWEKA MKAKATI WA KUWEZESHA MJUMITA KUENDELEA KUWAPATIA USHAURI WA KITAALAM BAADA YA UFADHILI WA MRADI WA MKAA ENDELEVU KUISHA

Katika kuhakikisha uendelevu wa shughuli za uhifadhi, uvunaji endelevu na biashara za mazao ya misitu baada ya ufadhili wa mradi wa Mkaa Endelevu kuisha; Wanavijiji wa vijiji 35 (Kilosa – 20; Mvomero -10 na Morogoro -5) wameweka mfumo/utaratibu wa kulichangia fedha shirika la MJUMITA liendelee na kujengea uwezo jamii kuhusu usimamizi endelevu wa misitu na biashara za mazao ya misitu. Katika mfumo huu kila kijiji kitachangia asilimia saba ya mapato yake yatakayotokana na kuuza kiwango cha uvunaji wa mkaa na mbao kwa mwaka.

Vijiji vilifikia uamuzi huo kupitia mikutano ya Halmashauri za vijiji na Mikutano mikuu ya vijiji chini ya ushauri wa Halmashauri za Wilaya zao. Baada ya mikutano ya vijiji mfumo huu unatakiwa kuidhinishwa na Halmashauri ya Wilaya ili utekelezaji kuanza. Hadi sasa Wilaya ya Morogoro imeshaidhinisha mfumo huu kuanza utekelezaji wakati wilaya za Mvomero na Kilosa ziko katika hatua za mwisho za kuidhinisha mfumo huu.

Kupitia mfumo huu vijiji vitanufaika na mambo yafuatayo:-

a) Kuhakikisha kwamba mifumo ya usimamizi endelevu, uvunaji endelevu na biashara za mkaa na mbao na utawala bora katika misitu iliyoanzishwa kijijini wakati wa utekelezaji wa Mradi wa Kuleta Mageuzi katika Sekta ya Mkaa Tanzania inakuwa endelevu. Hivyo; jamii kutokata tamaa ya kusimamia misitu yao kwa kuwa itapata motisha ya moja kwa moja kutokana na mapato na huduma zitakazotokana na usimamizi endelevu wa misitu ya jamii.

b) Kupata msaada wa haraka wa ushauri wa kitaalam kutoka MJUMITA kwani Halmashauri za Wilaya zina changamoto ya uhaba wa Maafisa Misitu.

c) Vijiji kusaidiwa kufanya ufuatiliaji na uhakiki wa hali ya msitu kwa kutumia picha za anga ili kuweka mipango ya kuthibiti ufyekaji na ukataji miti ovyo.

d) Vijiji kushauriwa kuhusu mwenendo wa kukidhi vigezo na masharti yote ya sheria, miongozo na sera za Misitu na Mazingira ili kuendelea kuwa na sifa za kumiliki misitu waliyomilikishwa.

e) Vijiji kushauriwa na kujengewa uwezo katika kuongeza thamani ya mazao ya misitu na kufanya biashara endelevu za mazao ya misitu.



*Mkutano wa kijiji cha Mlilingwa wilaya ya Morogoro kujadili na kupitisha mfumo wa vijiji kuchangia 7% ya mapato ya misitu ili MJUMITA iweze kuendelea kutoa huduma za kitaalam kuhusu uvunaji endelevu na Biashara za mazao ya misitu*

f) Kusaidiwa kuunganishwa na wafanyabiashara waaminifu wa mkaa na mbao wakati ambapo kijiji hakijafanikiwa kuvuna au kuuza kiwango chote cha uvunaji.

g) Wajumbe wapya wa Halmashauri ya kijiji, Kamati ya Maliasili, vikundi vya mbao na mkaa kupewa mafunzo ya usimamizi na uvunaji endelevu wa misitu.

h) Vijiji kuanzishiwa mfumo wa kieloctronic wa ukusanyaji na utunzaji wa takwimu sahihi za mauzo ya mazao ya misitu ili kuhakikisha uwazi katika ukusanyaji wa mapato.



*Kikao cha Wataalam Halmashauri ya Morogoro kuweka mikakati tayari kwa kuanza utekelezaji wa mfumo wa vijiji kuchangia 7% ya mapato ya misitu ili MJUMITA iweze kuendelea kutoa huduma za kitaalam kuhusu uvunaji endelevu na Biashara za mazao ya misitu.*



*Timu ya Wataalam Halmashauri ya Mvemero baada ya kikao cha kuweka mikakati ya kumalizia uanzishwaji wa mfumo wa vijiji kuchangia 7% ya mapato ya misitu ili MJUMITA iweze kuendelea kutoa huduma za kitaalam kuhusu uvunaji endelevu na Biashara za mazao ya misitu*

# Ufuatiliaji wa viwango ya ufyekaji wa misitu katika maeneo ya mradi- Nini Tulichojifunza

Katika juhudi za kuhakikisha maeneo ya misitu yanaendelelea kuhifadhiwa ndani ya vijiji, Mradi wa TTCS ulifanya ufuatiliaji katika kipindi cha mradi kwenye maeneo yote ya mradi. Hadi kufikia mwezi Mei 2019, mradi ulifanikiwa kuthibitisha kupungua kwa kiwango cha ufyekaji wa misitu katika vijiji vilivyokuwa vinashiriki Usimamizi Shiriki wa misitu, kuliko vijiji vilivyoko nje ya utaratibu huu. Kwa mfano katika kipindi cha 2016/2017, kiwango cha ufyekaji kilishuka kwa asilimia -1.38 katika vijiji 10 vya awamu ya kwanza ya mradi wa TTCS Wilayani Kilosa kiwango ambacho ni chini kwa asilimia 59 ukulinganisha na kiwango cha awali wakati mradi unaanza kwa mwaka 2010 hadi 2014.Pamoja na hayo, mradi umeendelea kuwa na jukumu la kufuatilia kiwango hichi katika mtizamo wa kujenga uwezo wa kitaifa na kuchangia katika utekelezaji wa mkakati wa MKUHUMI ngazi ya kitaifa na kimataifa.

## Vijiji gani vilihusika katika Ufuatiliaji huu?

Katika kipindi cha mwisho wa mwaka 2019, teknolojia kwa njia ya "remote sensing" ilitumika kubaini maeneo ambayo yameathirika na ufyekaji wa miti ili kusaidiana na jamii kuweka mikakati ya kuboresha usimamizi. Ufuatiliaji huu ulifanyika katika vijiji 30 vya mradi vikiwa Maharaka, Sewe kipera, Misengele, Kihondo Msongozi kutoka Wilaya ya Mvomero. Na vijiji vya Tununguo, Matuli, Lulongwe, Diguzi na Mlilingwa kutoka Wilaya ya Morogoro na vijiji vya Ulaya Mbuyuni, Ulaya kibaoni, Kigunga, Mfuluni, Gongwe, Rudewa gongoni, Unone, Mvumi, Ihombwe, Mhenda, Chabima, Kisongwe, Mbamba, Kitunduweta, Zombo, Dodoma Isanga na Nyali, Kisanga, madizini na Msimba kutoka WIlaya ya Kilosa. Wakati huo huo vijiji vilivyokuwa chini ya mradi wa AVA vilivyofanyiwa ufuatiliaji ni Magunga, Ndole, Difinga, Dibuluma, Msolokelo na Masimba.



*Baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Timu ya Doria kutoka Kijiji cha Msolokelo wakati wa kufuatilia maeneo yaliyobainishwa.*

## Nini tulichojifunza kupitia ufuatiliaji huu?

### *Shughuli za kilimo zinachangia zaidi ukataji wa miti*

Katika vijiji vya Mlilingwa na Msongozi, shughuli za kilimo zilifuatiwa na uchomaji wa mkaa. Baadhi ya maeneo yalioainishwa yalikuwa mbali zana kutoka vijijini jambo ambalo linaashiria hata timu za doria zinaweza zisifike mara kwa mara katika maeneo hayo Mfano katika vijiji vya Misengele na Sewekipera ambapo kuna umbali wa zaidi ya kilomita 15 kutoka vijijini.

*Picha ikionyesha ukataji wa miti hovyo nje ya eneo la hifadhi ya Kijiji cha Msongozi likitanguliwa na uchomaji wa mkaa na baadae kilimo*



### *Kukosa Motisha ya kusimamia misitu*

Ufuatiliaji huu ulibaini kwamba katika vijiji ambavyo havipati mapato ya kutosha kutokana na uwepo wa misitu yao hawana hamasa ya kusimamia vizuri na kufanya doria za mara kwa mara. Na hii inahatarisha misitu iliyopo. Mfano Kijiji cha Difinga kiliuza misitu michache iliyobaki kupitia kwa viongozi wao. Kamati za Maliasili hawana hamasa wala motisha ya kusimamia kwa nguvu kutokana na viongozi wao wa Kijiji wanavyo shindwa kuwa na utawala bora.

### *Maeneo yenye ufyekaji wa hivi karibuni*

Katika ufuatiliaji na kwa njia ya teknolojia ya setilaiti, timu ya watalamu ilibainisha maeneo 109 ya kufuatilia. Wakati wa kutembelea maeneo hayo mengi yalibainika kuwa na shughuli za hivi karibuni sana za kilimo mchanganyiko na mazao makuu yakiwa mahindi kwa sehemu kubwa, uwele, ufuta, mihogo, mbaazi, viazi vitamu, mbogamboga na bangi kwa wingi hasa katika vijiji vya Misengele na Sewekipera.

Zaidi ya maeneo 150 kati ya 190 yaliyobainishwa na kutembelewa yamefyekwa. Baadhi ya maeneo yaliyofekwa hawakupanda kitu kutokana na timu za doria kupita maeneo hayo kwa wakati na kuwaondoa wahalifu msituni mapema hivyo uoto ulikuwa umeanza kurejea. Kwa kutekeleza shughuli hii ya ufuatiliaji wa maeneo yaliyobainishwa kwa teknolojia ya satellite, mradi, na

### *Shughuli za ufyekaji nyingi hufanywa na wageni kutoka nje ya vijiji husika.*

Katika baadhi ya vijiji, shughuli za ufyekaji zilikuwa zinafanywa na watu kutoka vijiji vya jirani. Mfano katika vijiji vya Kigunga, Ulaya Mbuyuni, Mbamba, Ndole na Mlilingwa ambapo kwa Kijiji cha Mlilingwa, uharibifu ulikuwa unafanywa na watu kutoka Kijiji cha Kiwege, wakati Dodoma ISanga ulisababishwa na watu kutoka Masugu juu na wanadhani eneo bado ni la kwao.,

### *Ugawaji hovyo wa ardhi na viongozi wa vijiji*

Baadhi ya viongozi wa vijiji wasio waaminifu wanashirikiana na wakulima na kutoa ardhi katika maeneo ya hifadhi za misitu ya vijiji. Mfano katika kijijicha Difinga ambapo karibu eneo lote la Kijiji limefyekwa kwa ajili ya kilimo. Kamati za maliasili zimeelemewa



*Timu ya doria na wajumbe wa Maliasili kutoka Kijiji cha Tununguo*

wadau wa mradi walifanikiwa sana kujua visababishi vya ufyekaji wa misitu. Hata hivyo watu ama wahalifu waliokuwa wamepatikana wakati wa kutembelea maeneo walipewa adhabu kulingana na sharia ndogo za misitu wa Kijiji, wengine walipelekwa mahakamani na wengine waliondolewa msituni kama kule Mlilingwa kuondoa watu kutoka Kiwege, Msongozi, Diguzi na Matuli. Kwa wale viongozi kutoka Misengele na Sewekipera, walikubaliana kuwahusisha Mamlaka ya Wilaya ili kutumia polisi kufanya doria kwa wingi hasa kwenye yale maeneo wanapolima bangi.

Wananchi kupitia Kamati za Maliasili na timu za doria wanahamasishwa kuendelea kufanya doria na kusimamia misitu yao ili maeneo ya misitu yalindwe.



**Zaidi ya maeneo 150 kati ya 190 yaliyobainishwa na kutembelewa yamefyekwa**

*Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na wajumbe wa Doria kutoka Kijiji cha Mlilingwa wakati wa zoezi la ufuatiliajiwa maeneo yaliyofyekwa.*



Tanuri  la mkaa tayari kwa kuchomwa katika harakati za kufungua shamba katika Kijiji cha Msongozi

## Wabia wa Mradi

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Swiss Agency for Development and Cooperation SDC

SDC ni **Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi** (SDC). Ni Shirika la Kimataifa na Ushikiano nchini Uswisi. Mradi unafadhiliwa na SDC.
info@deza.admin.ch www.sdc.admin.ch

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

**Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG)** ni shirika lisilo la kiserikali lenye maono ya kuhifadhi na kurejesha misitu yenye bionauwai muhimu kitaifa na kimataifa. TFCG ndiyo mtekelezaji mkuu wa mradi huu wa CoForEST.
tfcg@tfcg.or.tz www.tfcg.org

MTANDAO WA JAMII WA USIMAMIZI WA MISITU TANZANIA
MJUMITA

**Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA)** ni Mtandao wa kitaifa wa vikundi vya jamii vinavyo shughulika na Usimamizi Shirikishi wa Misitu. MJUMITA ina jukumu la kuanzisha mfumo wa USMJ unaweza kujiendesha katika Mkoa wa Morogoro na kuwezesha jamii na kufanya ushawishi wa mabadiliko ya sera zitakazowezesha USMJ
mjumitaorg@mjumita.org www.mjumita.org

Mradi wa CoForEST unatekelezwa kwa kushirikiana na:

- Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa,
- Idara ya Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Raisi,
- Wizara ya Maliasili na Utalii,
- Halmashauri za Wilaya katika Wilaya saba,
- Sekretariat za Mikoa katika Mikoa mitano
- Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine,
- Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI)
- Chama cha Wanamisitu wa Africa (AFF)

Kwa taarifa Zaidi kuhusu mradi tafadhali tembelea :

- www.tfcg.org/what-we-do/develop/sustain-able-charcoal/
- https://www.instagram.com/sustainablechar-coaltz/
- Twitter-: CoForEST Project @CoforestP